

## Utupaji wa kuwajibika wa taka za vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vilivyozeeka na vilivyoharibika

Kipeperushi hiki kuhusu Taka za Kielektroniki kimeundwa kama sehemu ya Programu ya Elimu ya Mtumiaji ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya na kinawakilisha mtazamo wa sasa wa habari iliyopo kuhusu taka za kielektroniki nchini Kenya.

### Ufafanuzi wa taka za kielektroniki

Taka za kielektroniki ama Taka za Vifaa vya Umeme na Kielektroniki (WEEE) zinamaanisha vifaa vya umeme au vya kielektroniki vilivyotupwa.

### Aina ya taka za kielektroniki

Kuna aina mbalimbali za taka za kielektroniki kama ifuatavyo:

- Vifaa vikubwa na vidogo vya nyumbani
- Vifaa vya TEHAMA na vya mawasiliano ya simu
- Vifaa vya watumiaji
- Vifaa vya taa
- Zana za Umeme na Kielektroniki
- Vifaa mwanaserere vya starehe na vya michezo
- Vifaa vya matibabu
- Vyombo vya Ukaguzi na udhibiti
- Vigawaji atomatiki

### Hali ya Taka za Kielektroniki nchini Kenya

Utupaji wa taka za kielektroniki unaongezeka kwa haraka sana humu nchini hususan kutokana na utupaji wa taka za vifaa vya mawasiliano ya simu kama vile simu za mkono na vipuri vya kompyuta.

Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kufikia huduma za mawasiliano kwa kila mtu ili kupunguza tofauti iliyopo ya mfumo wa kidijitali. Miradi mbalimbali ya kimataifa pamoja na ile ya Serikali ya Kenya, imechangia pakubwa, ukuaji wa haraka wa sekta ya mawasiliano kwa kuwezesha mawasiliano, biashara na uuzaji wa vifaa vya mawasiliano kwa bei nafuu.

Kadhalika, vifaa vya umeme vilivyorekebishwa vimechangia pakubwa kuongezeka kwa taka za kielektroniki nchini Kenya. Sababu nyingine ni ongezeko la kila siku la mahitaji ya watumiaji huku wakiagiza vifaa vyenye mitindo ya kisasa na vya mawasiliano ya kisasa zaidi, hatua ambayo hatimaye husababisha kutupwa kwa vifaa vya kitambo zaidi.

Watumiaji hutupa vifaa vyao vya mawasiliano kwa njia mbalimbali kama vile kuwauzia marafiki pamoja na wanafamilia wengine, kuhifadhi, kuchoma na kutupa kama taka. Baadhi ya watumiaji huwacha vifaa hivyo katika nyumba zao kwa kuwa wanavithamini au kwa kukosa njia inayofaa ya kuvitupa. Njia hizi za kutupa taka hazifai.

Utupaji wa taka za kielektroniki ovyo ovyo ni hatari kwani huwa unaathiri vibaya mazingira na husababisha madhara makubwa kwa afya ya mwanadamu.

FOLD

### Hatari za aka za Kielektroni

Hatari hutoka kwenye vijenzi vinavyotumika kuunda vifaa hivyo kama vile risasi, zebaki, arseniki, kadimi, shaba, beriliamu, bariamu, na kromiamu, nikeli, zinki, fedha na dhahabu.

Wakati taka za kielektroniki zinapotupwa katika maeneo au mabiwi ya taka, mfumo wa usambazaji wa maji au kuingia hewani, huku ikiathiri pakubwa jamii inayoishi karibu na eneo hilo.

Baaadhi ya hayo, Kuna athari mbaya zaidi zinazotokana na kuendelea kupata viwango vya juu vya vijenzi hivi kwenye taka za kielektroniki ni kama zifuatazo:

**a) Athari za Kiafya:**

- Uharibifu wa mifumo ya neva ya sehemu za kuu na pembeni, mifumo ya damu na hata figo.
- Huathiri ukuaji wa ubongo wa mtoto.
- Sumu mbaya sana kwa afya ya mwanadamu.
- Uharibifu sugu wa ubongo.
- Matatizo ya kupumua na ngozi.
- Matatizo ya uzazi na ukuaji.
- Uharibifu wa mfumo wa kinga mwilini.
- Muingiliano wa homoni zinazodhibiti mwili.
- Kuvuruga utendakazi wa mfumo unaounda homoni.

**b) Athari za Kimazingira:**

- Uchafuzi wa hewa, maji na mchanga-udongo.

**c) Athari za Kijamii:**

- Katika mtazamo hasi, taka za kielektroniki huongeza gharama katika huduma ya afya.
- Katika mtazamo chanya, huongeza biashara isiyo rasmi pamoja na usimamizi wa taka za kielektroniki.

Taka za kielektroniki zinapotupwa kwa njia inayofaa huweza kuwa malighafi ya sekta mbalimbali za uchumi.

### Jinsi ya kupunguza athari mbaya za taka za kielektroniki

Kuna mikataba miwili mikuu ya kimataifa inayodhibiti usimamizi wa taka, hii ni pamoja na Mikataba ya Basel na Bamako. Kenya imejiunga na Mkataba wa Basel.

Mikataba hiyo inahitaji wanaotia saini kuhakikisha kwamba:

- Utoaji wa taka zenye sumu humu nchini umepungua kiasi, kwa kuzingatia sababu za kijamii, kiteknolojia pamoja na kiuchumi.

- Hatua zinachukuliwa ili kupunguza uchafuzi wa mazingira na athari zake za kiafya kadri iwezekanavyo hususan pale ambapo nchi inayotoa taka za sumu haina uwezo wa kiufundi, vituo muhimu, ama maeneo yanayofaa kutupa taka kwa namna inayofaa na itakayolinda mazingira.



FOLD



Hata hivyo, Kenya haina sera ya usimamizi wa taka za kielektroniki hususani ile inayoshughulikia utupaji/utumiaji upya wa taka za kielektroniki. Kwa kutokuwepo kwa sera kama hiyo, Mamlaka ya Mazingira nchini (NEMA) iliunda Ilani ya Kisheria Nambari 121 kuhusu Masharti ya Mazingira na Uratibu (Usimamizi wa Taka) 2006. Masharti hayo yanaelezea taka za kielektroniki kama taka zenye sumu - ikiwa ni pamoja na zile zenye chuma nyingi ndani - Zinazohitaji Kushugulikiwa kimaalum na kutupwa baada ya kuidhinishwa na Mamlaka.

Ukosefu huu wa njia muafaka za kutupa taka ulimaanisha kwamba hatua iliyopendelewa zaidi ilikuwa ni kuzipeleka taka mbali, huku kiwango kikubwa cha taka hizo kikiishia kutupwa kwenye sehemu za majalala ya taka.

Kadhalika, NEMA imeunda Mwongozo wa Usimamizi wa Taka nchini Kenya, ambao hatimaye unaandaa msingi thabiti wa kuundwa kwa masharti pamoja na sera ya taka za kielektroniki humu nchini.

Miongozo hiyo inatoa taarifa kuhusu jinsi ya kuendesha utaratibu wa kushughulikia pamoja na kutupa taka za kielektroniki zilizozalishwa na sekta mbalimbali pamoja na mfumo wa kutambua, kukusanya, kuteua, kujalalisha na kutupa taka za umeme na za kielektroniki. Kadhalika, wanatoa msingi wa uandalizi wa vifaa vya kisheria ili kuimarisha ushughulikiwaji wa taratibu hizo.

### Jitihada za Mamlaka ya Mawasiliano (CA) katika kushughulikia masuala ya usimamizi wa taka za kielektroniki

Katika jukumu lake kama msimamizi mkuu chini ya mfumo mpya wa kisheria kama ulivyo chini ya Sheria ya Mawasiliano ya Kenya (Rekebisho) 2013, Mamlaka inatambua kwamba taka za kielektroniki zina uhusiano mkuu kati ya uendelevu wa TEHAMA na mazingira. Katika jitihada za kushughulikia masuala ya taka za kielektroniki pamoja na kutangaza ukuaji kwenye sekta ya mawasiliano kwa kuimarisha ufikiwaji wa huduma za mawasiliano, Mamlaka hii ilitekeleza mipango ifuatayo: **Ushirikishaji wa mahitaji ya usimamizi wa taka za kielektroniki katika masharti ya kutoa leseni.**

FOLD

Sera ya TEHAMA ya Kenya 2019 inatambua hatari za taka za kielektroniki na taifa linatoa njia za uundwaji wa sera kamilifu kuhusu usimamizi wa taka za vifaa vya umeme na vile vya kielektroniki, kulingana na ushirikiano chanya na washikadau pamoja na uandaaji wa mifumo ya uratibu kati ya sekta ya umma, binafsi na zile zilizogatuliwa pamoja na mashirika ya kiraia.

Kadhalika, inatoa fursa ya uundwaji wa orodha ya uzalishaji wa taka za kielektroniki, ukusanyaji na ujalalishaji humu nchini na kushughulika ili kutambua na kuondoa vizingiti kuu katika utaratibu mzima wa ujalalishaji.

Kadhalika Serikali itatoa takrima kwa utumiaji mzuri wa taratibu zinazofaa ili kuhimiza kupunguza uwepo wa alama za kaboni, usimamizi bora wa kawi, ujalalishaji wa taka za kielektroniki, uhifadhi wa vyanzo vya maji, upandaji wa miti na ujalalishaji wa bidhaa za TEHAMA.

Zaidi ya hayo, Serikali itatoa takrima kwa wawekezaji na wabunifu wanaounda vituo vya uundaji wa mbinu za utupaji wa taka za TEHAMA pamoja na ujalalishaji utakaozingatia viwango vya ubora wa kimataifa vya vitakavyokubalika pamoja na mazingira.

Utekelezaji wa sera kama hizo utahakikisha kwamba waendeshaji wanawajibika zaidi katika ushughulikiaji wa taka za kielektroniki kwa kuhakikisha utumiaji salama wa vifaa vya kielektroniki na kuweka taratibu muafaka za kupunguza athari za kimazingira za taka za kielektroniki. Kwa sababu hiyo, huo mfumo mpya wa leseni uliotekelezwa mnamo 2008 unawahitaji wenye leseni "kuhakikisha kwamba mifumo/vifaa vilivyotolewa leseni havileti hatari ya kiafya, kimazingira ama kiusalama..."



### Uidhinishaji wa aina mbali mbali vya vifaa vya mawasiliano

Aina ya uidhinishaji wa simu za mkono inahakikisha kwamba kifaa cha mawasiliano sio na hakitakuwa na hatari ya kiafya na pia kinazingatia viwango vya ubora vilivyowekwa na Shirika la Viwango vya Ubora wa Bidhaa la Kenya (KEBS).

### Matumizi na uondoaji wa muundomsingi wa mawasiliano

Watoaji wa huduma za mawasiliano wanahimizwa kutumia kwa pamoja vituo vya mawasiliano na kufuata mahitaji ya Sheria ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira (EMCA) ya 1999, inayoagiza utambulisho na utekelezaji wa hatua za kupunguza makali katika matumizi na uondoaji wa muundomsingi wa mawasiliano.

### Mkataba wa Makubaliano kati ya Mamlaka na NEMA

Mkataba wa Makubaliano (MOU) unaitaka Mamlaka hii pamoja na NEMA kushirikiana katika uundaji wa sera, miongozo na vyombo vingine vinavyohitajika kwa ajili ya utupaji wa taka za kielektroniki nchini Kenya unaofaa.

### Ushauri wa washikadau kuhusu usimamizi wa taka za kielektroniki

Kwa lengo la kuchochea shughuli za maendeleo ya mfumo wa usimamizi wa taka za kielektroniki nchini Kenya, Mamlaka hii inaendelea kuwashirikisha washikadau wakiwa ni pamoja na NEMA katika mipango itakayoimarisha utupaji salama wa taka za kielektroniki humu nchini.

FOLD FOLD FOLD

## Mradi wa Madaraka

Lengo la Mradi wa Madaraka ni kuunda kompyuta humu nchini kwa nia ya kuziuza kwa bei nafuu. Mradi huu ulianza wakati kukiwa na hofu kubwa kwamba Kenya imekuwa jalala la taka za kielektroniki kwa umbo la kompyuta zilizopitwa na wakati na maunzi magumu na maunzi laini mengne.

Mamlaka ilitoa kitita cha Shilingi za Kenya Milioni 10 kwa asasi mbili za kiteknolojia ili kugharimia uundwaji wa kituo kilichopendekezwa cha uundaji wa kompyuta humu nchini chini ya Mpango huu wa Madaraka.

## Jinsi ya kuwajibika wakati wa kununua, kutumia, kutumia upya na kutupa kifaa cha TEHAMA

Mashirika na watumiaji wanaopenda kuwajibika wakati wa kununua, kutumia, kutumia upya tena pamoja na kutupa TEHAMA wanafaa;

a) Kutoa mchango wa kifaa kwa watumiaji wengine ama mashirika. Hatua hii itaongezea thamani ya maisha ya bidhaa hizo na kuviondoa katika mfumo wa usimamizi wa taka za kielektroniki kwa kipindi kirefu k.v kwa shule na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Kifaa kilichotolewa kama mchango kinafaa kuwa katika hali nzuri ya kuweza kutumika.

b) Kutenganisha taka zote za umeme na zile za kielektroniki kutoka kwa taka nyinginezo pamoja na taka za nyumbani wakati kutupa taka hizo. Taka za kielektroniki hazipaswi kabisa kutupwa pamoja na taka pamoja na uchafu wa nyumbani.

c) Kutupa taka za kielektroniki kupitia mashirika yaliyo na leseni ya kutupa taka hatari.

d) Wakati unaponunua bidhaa za kielektroniki, chagua zile ambazo:
   - Zimeundwa kwa kutumia vijenzi vichache mno vya sumu.
   - Zinatumia vitu vilivyojalalishwa.
   - Zinahifadhi kawi ndogo.
   - Zimeundwa kwa njia ambayo ni rahisi kuboresha ama kutenganisha.
   - Zinazotumia vitu vichache kupakia.
   - Zinatoa fursa ya ukodishaji ama chaguo la kurudisha baadaye.
   - Zimeidhinishwa na mamlaka za usimamizi.
   - Zinaweza kusasishwa ziwe kompyuta ama bidhaa nyingine za kisasa badala ya kununua bidhaa nyingine mpya.




## Ni wapi na jinsi gani unavyoweza kutupa taka za kielektroniki nchini Kenya

Zifuatazo ndizo njia sahihi unazoweza kutumia ili kutupa vifaa vyako vya mawasiliano:

1. Waundaji wa Vifaa vya TEHAMA: Baadhi ya waundaji wa vifaa vya mawasiliano wameandaa mpango mpana wa kuchukua vifaa vya kitambo na visivyotumika. Tafuta taarifa kutoka kwa waundaji wa vifaa ili kujua iwapo vina "Mpango wa Kurudishwa Baada ya Kutumika" utakaowawezesha kutupa vifaa hivyo kwa njia inayofaa.
2. Peleka kwa kampuni iliyopewa leseni ya kujalalisha taka ambayo inatawanya na kushughulikia taka za kielektroniki. Hizi ni pamoja na kampuni zifuatazo:

**a) Computer for Schools Kenya**
Simu: +254 020 60919, 0733 986558
SLP 48584
00100
Nairobi, Kenya

**b) WEEE Centre**
National Youth Service, Ruaraka,
Barabara Kuu ya Thika
SLP 48584
00100,
Nairobi, Kenya
Simu: +254 (0) 20 2060921,
Kipepesi: + 254 (0) 20 2060920
Baruapepe: info@weeecentre.com

**c) WEEE Centre Collection Point**
Government Training Institute,
Barabara ta Vanga kando ya Barabara ya Nyerere,
SLP 84027 - 80100
Mombasa, Kenya
Simu: + 254 041 2230717
Simu ya Rununu: + 254 727637075
Baruapepe: mombasa@weeecentre.com

**d) East Africa Computer Recycling Ltd**
Njia ya Makaburini,
Barabara ya Malindi-Mombasa
Simu: +254 715 036 515, 0729 308 221
SLP 1039-80100
Mombasa, Kenya

**e) Vituo vyote vya ukusanyaji na mipango ya kuchukua tena baada ya matumizi iliyopewa leseni**



## Ungependa kujua mengi?

Kwa taarifa zaidi kuhusu taka za kielektroniki au aina nyingine yoyote ya ulinzi wa kimazingira unaoambatana na vifaa vya mawasiliano, tafadhali wasiliana na idara ya:

**Idara ya Masuala ya Watumiaji na Umma**
**Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya**
**SLP 14448, Westlands,Nairobi, Kenya 00800**
**Baruapepe: CPA@ca.go.ke; chukuahatua@ca.go.ke**
**Simu: 020-4455555, 0714-444555, 0737-445555**

**Unahitaji kufahamu zaidi?**

Kwa habari zaidi kuhusu mada iliyopo hapo juu au sehemu nyingine yoyote ya afya na usalama wa mitambo ya mawasiliano, tafadhali wasiliana na:

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA
*OPENING YOUR WORLD*

**Head Office**

CA Centre, Waiyaki Way, P.O. Box 14448, Nairobi 00800
Mobile: 0703042000,
Complaints: chukuahatua@ca.go.ke
Talk to us : pea@ca.go.ke,info@ca.go.ke
020-445 5555, 0714 455 555, 0737 455 555

**CA Western Regional Office**
1st Floor KVDA Plaza
P.O. Box 2346
Eldoret 30100
Mobile: 0703042105
Email: wro@ca.go.ke

**Central Regional Office**
Ground Floor, Advocates Plaza
P.O Box 134
Nyeri 10100
Mobile : 0703042181
Email : cero@ca.go.ke

**CA Coast Regional Office**
3rd Floor, NSSF Building
P.O. Box 8041
Mombasa 80100
Mobile: 0703042152
Email: cro@ca.go.ke

**Nyanza Regional Office**
2nd Floor Lake Basin Mall,
P.O Box 2016
Kisumu 40100
Mobile: 0703042130
Email: nro@ca.go.ke

**Ilani ya kujitoa hatarini:** Huku kila jaribio likiwa limefanywa ili kuhakikisha kuwa habari iliyojumuishwa katika hati hii ni sahihi, imekusudiwa TU kuwa kama mwongozo wa kuelekeza utendakazi salama wa mitambo ya mawasiliano na haipaswi kuchukuliwa kama (au kutumika badala ya) ushauri wa kisheria. Kwa hivyo,

Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya haitakubali kosa lolote kwa matokeo ya hatua zozote zilizochukuliwa, au maamuzi yaliyotolewa kwa misingi ya taarifa iliyotolewa.

CA/PEA/CEP/KIS/B/16/2020

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA

www.ca.go.ke

# TAKA ZA KIELEKTRONIKI



CHUKUA HATUA
PATA HUDUMA YA MAWASILIANO UNAYOSTAHILI